www ppmedia com

# Alasiri Online

ISSN 0856 Na. 001 Alhamisi 4 Aprili, 2019 Tanzani 500/- Kenya 50/-



# WONDER KUPAKUA KITU MWEZI HUU

## Muumini ajikusanya

## Diana Kimary ameamua kuvunja ukimya

## Sikia tambo za Kingwendu

## Duma: Mdogo mdogo ndio mwendo

## Irene Paul amepachikwa haya

# VOICE WONDER
## KUPAKUA KITU MWEZI HUU




**Na Anaeli Mbise**

MWANAMUZIKI Voice Wonder amekwama kurejea kwenye gemu kwa muda aliokuwa amejipangia akidai kwamba ni kutokana na sababu zilizo juu ya uwezo wake.


Akizungumza na Alasiri Online Wonder amesema alikuwa amepanga kuanza kufanya vitu Januari mwaka huu akiwa na vibao viwili, lakini ameahirisha hadi mwezi huu na atatambulisha kibao kimoja tu kiitwacho Kitu Kamba.

"Katika maisha unaweza kupanga jambo lako, lakini Mungu akalibadilisha ndivyo ilivyotokea kwangu, lakini sasa nitarejea rasmi kwenye gemu mwezi ujao (Aprili) nikiwa na Kitu Kamba nilichomshirikisha Barnaba," amesema Wonder.

Aidha mwanamuziki huyo amewaomba radhi mashabiki waliokuwa wakisubiri ujio huo kwa hamu na kuwataka wamvumilie hadi Aprili atakapoitambulisha ngoma mpya.

Wonder ameongeza kuwa muziki wa siku hizi umekua sana kibiashara, hivyo msanii anatakiwa atunge mashahiri ya kueleweka kwa ajili ya ushindani.

HABARI KITAIFA



# Muumini ajikusanya

Na Mary Kadoke

MWINJUMA Muumin yuko kwenye mkakati wa kuhakikisha bendi ya Double M Extra inarudi jukwaani tena katika viwango kama ilivyokuwa mwaka 2002.

Akizungumza na Alasiri Online amesema anachokifanya sasa ni kuweka sawa mkakati huo na kuona kuwa anarudisha kundini wanamuziki alioanza nao wakati huo na kuiweka bendi matawi ya juu.

"Kwa muda mrefu nimekuwa na wanamuziki wachanga, lakini sasa nimeanza kuwarudisha mwimbaji Bashir Uhadi, mpiga solo Rashid Sumun na mpiga drums Michale Liloko, ninaendelea kusaka wengine," amesema Muumin.

Amesema licha ya kwamba kwa sasa bado vyuma vimekaza, ana uhakika kufikia katikati ya mwaka huu bendi hiyo itakuwa tayari imeimarika ikiwa na wanamuziki wachanga na wakongwe. Bendi hiyo ilitamba na ngoma kama Tunda, Ndugu Lawama na Mgumba.

# Kimary ameamua kuvunja ukimya

Na Mary Kadoke

MUIGIZAJI Diana Kimary ameamua kuvunja ukimya kwa waigizaji wenzake na kuwataka kupata muda wa kumshukuru Mungu kwani miongoni mwao wamekuwa ni watu wa kufanya hivyo kwa matukio.


Amesema hayo alipofanya mazungumzo na Alasiri Online akishangazwa na wale wanaoamka siku za ibada na kukimbilia makazini badala ya nyumba za ibada.

"Hakuna kitu kibaya kama kujisahau, mastar wengi huona bora aamke kwa muda atakaotaka na baadaye kwenda kazini," amesema.

"Ni muhimu kujenga mahusiano mazuri na Mungu filamu zetu zinawezaje kusonga mbele wakati hatumpi nafasi aliyetuumba," amesisitiza.

Jina la Diana liliwika zaidi baada ya kuonesha umahiri wake wa kui-





# Irene Paul amepachikwa haya

Na Mary Kadoke

WATU wanaweza kupachika sifa ambazo hustahili na kwa kuwa tu wamebeba hisia potofu dhidi yako, hivyo ndivyo kwa mwigizaji Irene Paul, ambaye amebandikwa wasifu wa kuringa.

Akizungumza na Alasiri Online, msanii huyo amesema kujitenga kwake kutokana na bali woga wa kujiingiza kwenye makundi ambayo mwisho wa siku huleta maadui na si marafiki, kumemfanya aonekane anaringa.

Akieleza zaidi kuhusu hilo amesema kutulia nyumbani na sio kuzurura majumbani mwa watu ni kitu ambacho alijifunza kutoka kwa wazazi wake hivyo tabia hiyo ndiyo atakayoendelea nayo katika familia yake.

"Siringi basi tu ni kwamba sipendi kujichanganya kwenye makundi ambayo mwisho wa siku yatazuka mambo ya kusutana," amesema.

"Kitu ambacho ninakiogopa sana. Nadhani ni utaratibu niliourithi tangu nikiwa mdogo nyumbani kukaa na kutulia nyumbani," amesema mkali huyo wa filamu ya Love and Power.



# SIKIA TAMBO ZA KINGWENDU

Na Anaeli Mbise

NYOTA wa vichekesho Kingwendu ametaja vigezo anavyozingatia kabla ya kushirikishwa kwenye video za nyimbo za wasanii, kundi au bendi.

Akizungumza na Alasiri Online, Kingwendu amesema siyo kila mchekeshaji anatakiwa kuchukuliwa poa kutokana na kazi anazofanya, hivyo lazima sasa aweke vigezo na masharti kama mtu anataka kumtumia.

"Kwanza kabisa ni mshiko ujumbe wa wimbo na pia ninaangalia kama msanii anajulikana au hajulikani, vinginevyo sitaki kushirikishwa," amesema Kingwendu.

Msanii huyo anayetamba na wimbo wa Ukerewe amesema yeye ni kivutio katika video, hivyo hatajishusha thamani ili mwingine afaidike.

Kingwendu amesema muziki ni biashara, hivyo anayemfuata ili kushirikishwa katika video ni lazima awe amejipanga vizuri ili baadaye wasisumbuane.

HABARI KITAIFA

# Duma: Mdogo mdogo ndio mwendo



Na Mary Kadoke

MUIGIZAJI Duma amefunguka kuwa katika maisha si lazima uanze na mtaji mkubwa ili kufanikiwa, kidogo kinapoongezewa thamani siku zote huleta faida.

Amesema hayo alipofanya mazungumzo na Alasiri Online akisisitiza watu kufanya kazi na kuachana na tabia ya kuombaomba.

"Ukitaka kufanikiwa usisubiri kuanza na mambo makubwa, bali unaweza kuanza na hicho kidogo ulichonacho kwani hata mbuyu ulianza kama mchicha," amesema.

"Maisha mazuri hayaji kwa kulalamika na kuomba omba watu wakusaidie bali yanakuja pale ambapo unajitoa na kupambana kuhakikisha kila kitu kinakaa sawa," ameongeza.

Duma ni staa anayetikisa Bongo Movie kwa sasa asilimia kubwa amekuwa akishindanishwa na Gabo kwenye tuzo mbalimbali kutokana na ubora wa kazi zao.

Filamu aliyowahi kuachia na ikafanya vizuri zaidi ni Nipe Changu aliyoiachia Julai mwaka jana.